# CLASS 7 MID TERM 3 DECEMBER 2021
# KISWAHILI

MUDA: Saa 1 dakika 40

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

Ni jambo ambalo ni __1__ kama paji la uso kwamba uhalifu unazidi __2__ katika pembe zote ulimwenguni. Walimwengu wamejipata hali taabani. Kila kukicha, wanakumbwa na tisho maishani mwao. Tisho hili __3__ kwa wanyama. La hasha! Linatoka kwa binadamu wenzetu. Kamwe, ulimwengu __4__ mahali salama tena pa kuishi. Baadhi ya binadamu wamegeuka kuwa hayawani kuanzia vijijini hadi majijini. Kuna wanyama __5__ kwenye ngozi na rangi za __6__. Hata wanazo lebasi za insi. Kila wakati __7__ nao mahali popote __8__ ofisini, mikutanoni, maabadini, magarini na kila mahali.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. fiche | B. shahiri | C. bayana | D. wasiwasi |
| 2. | A. kukata mizizi | B. kukita mizizi | C. kukata njia | D. kukata kalima |
| 3. | A. linatokea | B. huonekana | C. hutokana | D. halitoki |
| 4. | A. si | B. ni | C. na | D. kwa |
| 5. | A. akali | B. kichele | C. sufufu | D. kidogo |
| 6. | A. binadamu | B. ngombe | C. wanyama | D. ndege |
| 7. | A. tunaonana | B. tunabishana | C. tunakimbizana | D. tunatangamana |
| 8. | A. maadamu | B. mathalani | C. madhali | D. ingawa |

Katika siku za __9__ karibuni, aliishi mtoto wa kike kwa jina sitaki. Aliishi na wazee __10__ katika kijiji cha Pakata. Kijiji hiki kilijaa watu __11__ ambao walipenda mno raha na starehe __12__ la jasho __13__ la kujituma. Muda wao __14__ ulitumiwa kujikalia shambiro katika gumzo na kucheza bao __15__ maeneo ya burudani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. hapa | B. hii | C. hivi | D. huku |
| 10. | A. zake | B. wake | C. wao | D. zao |
| 11. | A. wachapakazi | B. wenye bidii | C. wangwana | D. wazembe |
| 12. | A. wasijue | B. wakiwa | C. wakifahamu | D. wakiona |
| 13. | A. na | B. ila | C. wala | D. pengine |
| 14. | A. mwingi | B. kwingi | C. nyingi | D. pengi |
| 15. | A. katika | B. kwenyewe | C. hapa | D. vilevile |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

16. ***Upi ni wingi wa:***
Mkunga alimvua mkunga akanyang'anywa na sokwe.
A. Mkunga aliwavua mikunga akanyang'anywa na sokwe.
B. Mikunga walivua wakunga akanyang'anywa na masokwe.
C. Wakunga waliwavua mikunga wakanyang'anywa na masokwe.
D. Wakunga walivua mkunga wakanyang'anywa na sokwe.

17. Ni sentensi gani iliyotumia silabi kwa ya kumiliki?
A. Mariera aliendа kwao kuwajulia hali wazee wake.
B. Kwa Tomaso ni huko kwenye miembe mingi.
C. Tutamtembelea daktari kwa matibabu.
D. Sikujua kuwa kuongea kwangu kwa sauti kungemwamsha mtoto.

18. Ni neno lipi limeambatanishwa kwa maana yake ifaavyo?
A. Korija - Kundi la vitu kumi.
B. Jozi - Kundi la vitu ishirini.
C. Mwongo - Kundi la miaka mia moja.
D. Pea - Kundi la vitu viwili.

19. ***Na imetumikaje katika sentensi hii:***
Naomba tuonane wiki ijayo na mwalimu.
A. wakati uliopo, pamoja na.
B. hali isiyodhihirika, pamoja na.
C. ufupishaji wa nafsi, umilikaji.
D. mnyambuliko, wakati uliopo.

20. ***Chagua kauli ya kutendewa ya:***
Rudi alichukua gari la Diru.
A. Gari la Diru lilichukuliwa na Rudi.
B. Gari lilichukuliwa kwa Rudi na Diru.
C. Diru alichukuliwa gari na Rudi.
D. Diru alichukua gari la Rudi.

21. ***Jaza pengo kwa kihusishi mwafaka:***
Wanafunzi wamo_____ darasa.
A. ndani kwa B. katika
C. kwenye D. kwa

22. Mwalimu mkuu ni _____ wale watakaohojiwa kesho.
A. mbali na B. baina ya
C. baadhi ya D. miongoni mwa

23. Mtu anapowaaga wengine pasi na matarajio ya kukutana hivi karibuni, husema?
A. Alamsiki. B. Kwa heri ya kuonana.
C. Buriani. D. Kwaheri kabisa.

24. Mtu mjuzi wa kutengeneza vitu vya fedha huitwa.
A. Sonara B. Mhunzi
C. Mjumu D. Mjume

25. ***Kanusha:***
Wangeonana wasingepigiana simu.
A. Wasingeonana wasingepigiana simu.
B. Wasingalionana wasingalipigiana simu.
C. Wasingalionana wangalipigiana simu.
D. Wasingeonana wangepigiana simu.

26. ***Teua kielezi katika sentensi hii.***
Mwanafunzi aliye na bidii sana ni Marwa.
A. aliye B. sana C. bidii D. na

27. Chagua sentensi iliyo sawa kisarufi.
A. Ndugu zangu walienda dukani.
B. Ndugu wangu walienda dukani.
C. Ndugu zangu walienda katika dukani.
D. Ndugu wangu walienda kwenye dukani.

28. Chagua sentensi inayoonyesha matumizi ya **"karibu"** kwa dhana ya umbali.
A. Alinyongwa na maneno karibu aanguke.
B. Darasani mna wageni karibu watano.
C. Gari liliharibika karibu na soko.
D. Mechi itaisha hivi karibuni.

29. Aliniita a**ka**nituma dukani. **Ka** iliyotumika inaonyesha dhani gani?
A. Kuonyesha mnyambuliko wa matukio.
B. Kuonyesha amri kwa mtenda.
C. Kuonyesha sababu ya kitendo.
D. Kuonyesha mfuatano wa matukio.

30. Onyesha sentensi yenye maelezo mwafaka.
A. Kaptula ni ugonjwa wa tumbo la kuendesha.
B. Malale husambazwa na mbu.
C. Kichocho huenea sana katika vyakula.
D. Homa ya manjano hutibiwa na ndorobo.

***Soma ufahamu huu kisha ujibu maswali 31 - 40***

Kwa yakini usalama katika nchi yetu unazidi kudorora kila uchao kila mmoja wetu anafadhaika kwa fadhaa na wahaka. Sote tuko <u>roho mkononi</u>. Kila mtu anapopiga milundi mtaani au mahali popote pale anaweza kuvamiwa na kuporwa. Kitendo cha kukenua kinywa kwa mzubao ni kuwa wengine huporwa na hata kuvamiwa mchana mwia ambapo jua limemwagа na kumwaya miale yake. Kwa hakika wananchi wengi hapa taifani wanaishi aushi za hatihati na kitete.

Aidha wapo wengine ambao hupika majungu kwa kuwasafirisha wenzao jongomeo bila nauli wala mizigo. Aghalabu, nina hakika kuwa amesikia redioni, au kutazama runingani ama hata kusoma magazetini kuwa watu kadha wa kadha wamenyakuliwa na mauko kutokana na uhasama waliokuwa nao. Kusema yakini, ni ngumu kumwaamini mtu yeyote. Haya ni kutokana na watu wazima na hata watoto vikembe kutekwa nyara. Hawa malaika huingia mtegoni madhali watekanyara wana mwao kuwa hawa ni windo rahisi kwani huweza kughulibiwa bila tashnishi.

Kwa kuwa watekaji nyara faradhi waamrishe wapewe ghawazi, aila za waliotekwa nyara huachwa wakiwa na kiwewe si kuduchu. Unaweza kupata kuwa hata baada ya mwezi mmoja ama zaidi, mja fulani hajapatikana wala. Kuachiliwa huru kwa kweli, jambo kama hili ni la kuatua moyo.

Licha ya usalama wetu kuzidi kudidimia dididi, ni sharti serikali izingatie suala la kuwahakikishia wananchi usalama wao maadamu hatuwezi katu kuishi maisha kama haya. Taraa, kitendo kinaporipotiwa katika kituo cha polisi, lazima kishughulikiwe mapema na wahalifu watiwe mbaroni. Wananchi nao wapige ripoti vituoni punde tu vitendo vya uhalifu vinapoonekana. Sote tutakapofanya hivyo, tutakuwa tukiiauni sana serikali yetu na taifa kwa ujumla.

Fauka ya hayo, sote tunafaa kupendana na kuenziana kama mboni za macho yetu. Tunafaa tushirikiane bega kwa bega zaidi ya kiko na digali ama jembe na mpini. Sote tukipendana na kuavizana katika wasaa wa shabuka na matatizo, hatuwezi kamwe kuoneana kijicho au kuchukiana bure bilashi. Ni faradhi tuzike ukabila na chuki katika mara ya liliwala. Tusipojifunza kuishi kwa utengamano na kwa amani, mambo yataishia kuenda zigizagi. Endapo tutaishi kama ndugu itakuwa adimu sana <u>bamthili</u> ya kaburi la baniani kupikiana majungu. Wananchi wanafaa kufahamu kuwa mbogo mwenda pweke ni windo rahisi la simba. Halikadhalika kofi hazilii ila kwa vitanga viwili.

Serikali inafaa kujaribu kadri ya uwezo wake kuwapa vijana amali. Hii ni kwa sababu utapata kuwa vijana ni watu ambao hutenda uhalifu madhali hawana lolote la kuwashughulisha. Hivi ni kusema kuwa endapo watapata chochote cha kuwashughulisha basi, watawazia namna ya kujibwesha na kukoma kujitosa katika vitendo hivyo benibeni.

**31.** Kwa mujibu wa aya ya kwanza, ni kweli kusema kuwa
- A. hakuna usalama kabisa nchini.
- B. viwango vya usalama vinazidi kuenda chini.
- C. viwango vya usalama vinazidi kuimarika.
- D. viwango vya usalama vinazidi kuwa afadhali.

**32.** Ni nini maana ya kuwa <u>roho mkononi</u>?
- A. kuhangaika.
- B. kuwa na upweke.
- C. kuwa na huzuni nyingi.
- D. kuwa na wasiwasi na woga mwingi.

**33.** Kulingana na ufahamu ni sahihi kusema kuwa watu wengine
- A. huibiwa mchana peupe.
- B. hupigana na wawaibiao.
- C. si rahisi kuwaibia.
- D. huwaripoti wanaowaibia kabla ya kuibiwa.

**34.** Mwandishi ana hakika kuwa msomaji amepata habari kuhusu uhalifu kupitia vyombo vyote hivi ila

A. magazeti B. runinga C. rununu D. redio

**35.** Watu wengi wanaaga dunia kutokana na nini kwa mujibu wa aya ya pili?
- A. Magonjwa yaliyoathiri afya zao.
- B. Uadui baina ya wanadamu.
- C. Ajali za barabarani zilizozidi.
- D. Amani na utengemano baina ya watu.

**36.** Wanatekwa nyara hasa ni akina nani?
- A. Akina mama na wazee.
- B. Vijana na watoto.
- C. Watoto na wasichana pekee.
- D. Watu wa umri wowote.

**37.** <u>Didimia dididi</u> ni tamathali gani ya lugha

A. kiigizi B. kiingizi

C. takriri D. tanakali

**38.** Wananchi wanahimizwa kufanya nini katika aya ya nne?
- A. Wawakamate wahalifu.
- B. Wawateketeze wahalifu.
- C. Wawaripoti wahalifu.
- D. Wawachunguze wahalifu.

**39.** Ikiwa wananchi wataishi kama ndugu
- A. watu wataishi kwa kusaidiana.
- B. uadui utazidi na watu watauana.
- C. serikali itawasaidia wote.
- D. polisi watawashika wahalifu wote.

**40.** Katika aya ya mwisho, serikali inahimizwa
- A. iwatie mbaroni wahalifu.
- B. iwape vijana kazi ili wajiendeleze.
- C. ihimize ushirikiano baina ya watu.
- D. iwape watu nyenzo za kuwaunganisha watu.

***<u>Soma ufahamu huu kisha ujibu maswali 41 - 50</u>***

Mwendazake baba yangu alikuwa mtu wa ajabu sana. Hakusoma zaidi ya darasa la saba lakini falsafa na hekima aliyokuwa nayo ingekustaajabisha hata wewe msomi. Awali ya yote, alikuwa mtu na utu wake. Daima alikuwa tayari kutenda haki. Fauka ya hayo alikuwa tayari kukuambia ukweli hata uwe mchungu kama shubiri.

Tabia yake hiyo ya kujieleza bila kificho ilimvunia mahasimu lukuki bin lufufu. Aliowapa kweli iliyo chungu walimchukia hadi na kumpangaza majina yasiyoandikika wala kutamkika kadamnasi.

Kati ya tabia zake zilizomtafautisha na waja wengine ni ukarimu. Tangu nilakiwe hapa duniani sijaona mtu kama yeye. Alikuwa tayari kukupa kibaba cha mwisho cha unga na yeye alalie mate. Roho yake ilikua nyeupe pepepe! Na weupe wa roho yake ulidhihirika kwa vitendo. Aliwapenda watu wote. Msemo wa adui mpende aliushika madhubuti.

Alinifunza kuwa ni rahisi kumpenda akupendaye lakini kitendawili kigumu ni kuwapenda wanaotuchukia. Tunapowapenda wanaotupenda hatuwi tofauti na watu wengine. Hata Idi Amin aliyeua waganda zaidi ya nusu milioni alikuwa na wandani wake aliowaenzi utu wa mtu unakamilika pale anapoweza kuwaonyesha mapenzi wale wanaomchukia.

Baba alinifunza mengi alipokuwa hai. La kwanza alilonifunza ni kuwa linalowezekana leo lisingoje kesho. Tabia hii ya kuweka mambo kiporo imechangia pakubwa katika hali duni ya maisha ya waja wengi. Pili hakuchoka kuniusia kuwa bidii ndiyo kurunzi ya mustakabali wa mja. Kwake yeye bidii huzaa ukakamavu nao ukakamavu huleta fanaka siku za usoni. Lakini la muhimu zaidi alilonifunza baba ni kuwa ukitaka kuishi maisha ya fanaka; raha mustarehe kama Sultan bin Jerere, usikope wala usikopeshe. Ukiweza kumsaidia mtu, msaidie tu. Kumpa mwenziwe si kutupa. Unapotoka asubuhi kuenda kutafuta riziki, ukipata shukuru, ukikosa usikufuru. Kukopa hudhalilisha. Hukufanya ukawa ombaomba hususan unapoifanya tabia. Ni nani asiyejua kuwa tabia ni ngozi ya mwili?

Pengine hatukubaliana na falsafa ya baba, lakini ukipiga durubini utagundua kuwa kuna ukweli fulani katika maneno yake. Ni nani aliye na raha? Anayedaiwa kope si zake au asiye na deni hata moja?

**41.** Jambo lililomfanya babake mwandishi kuwa mtu wa ajabu ni?
A. Kutosoma kwake.
B. Hekima aliyokuwa nayo.
C. Kustaajabisha hata wasomi.
D. Tabasuri aliyokuwa nayo ingawa hakusoma sana.

**42.** Tabia gani ya babake mwandishi iliyomzolea maadui wengi?
A. Kutenda haki.
B. Kusema ukweli bila kuficha.
C. Kujieleza bila kujali.
D. Kusema ukweli ulio mchungu.

**43.** Ni nini maana ya kulalia mate?
A. Kulala bila kula chochote.
B. Kulala palipotemwa mate.
C. Kutema mate kabla ya kulala.
D. Kulala kabla ya kulala.

**44.** Ni vigumu
A. kuwapenda wanaotupenda.
B. kuwachukia wanaotupenda.
C. kuenzi wanaotuchukia.
D. kutopenda wanaotupenda.

**45.** Ni maneno mangapi mwandishi aliyojifunza kutoka kwa baba yake?
A. Manne B. Mawili
C. Matano D. Matatu

**46.** Kulingana na makala, la muhimu zaidi mwandishi alilojifunza kutoka kwa baba yake ni?
A. Usikope wala usikopeshe.
B. Kopa lakini usikopeshe.
C. Ili uishi kwa raha usikope wala usikopeshe.
D. Ukikopa lipa mara moja.

**47.** "Tabia ni ngozi ya mwili." Ni msemo wenye maana kuwa
A. ukizoea jambo fulani, kuliacha ni vigumu.
B. ukianza kukopa mwisho utazoea.
C. tabia ni kama kiungo cha mwili.
D. mwili wa mtu lazima uwe na ngozi.

**48.** Baba yake mwandishi si kama watu wengine kwa sababu ya
A. hekima B. ukarimu wake
C. tabia yake D. falsafa

**49.** Mwandishi anasema kuwa;
A. hataona mtu kama baba yake.
B. duniani hakuna mtu kama baba yake.
C. tangu azaliwe hajamwona baba yake.
D. tangu azaliwe duniani hajaona mtu kama baba yake.

**50.** Kichwa mwafaka cha makala haya ni:
A. Mwendazake baba yangu.
B. Mtu wa ajabu.
C. Maajabu ya baba.
D. Falsafa za baba.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com